TANGAZO LA SERIKALI NA. 311 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA KODI YA MAPATO,

(SURA. 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

## AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA MAPATO KATIKA MRADI WA UKAMILISHAJI WA KAZI ZA UKARABATI WA MTAMBO WA KUSAFISHIA MAJI KATIKA MITAMBO YA WAMI-CHALINZE, UJENZI WA MTANDAO MKUBWA NA MDOGO WA BOMBA LA USAMBAZAJI MAJI NA UJENZI WA TENKI KUU ZA KUHIFADHIA NA KUSAMBAZA MAJI KATIKA VIJIJI VYA CHALINZE KWA KAMPUNI YA AFCONS INFRASTRUCTURES LIMITED YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Kampuni kwenye mradi wa Mradi Wa Ukamilishaji Wa Kazi za Ukarabati wa Mtambo wa Kusafishia Maji Katika Mitambo ya Wami- Chalinze, Ujenzi wa Mtandao Mkubwa na Mdogo wa Bomba la Usambazaji Maji na Ujenzi wa Tenki Kuu za Kuhifadhia na Kusambaza Maji katika Vijiji vya Chalinze kwa kampuni ya Afcons Infrastructures Limited ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tangu tarehe 26 Februari, 2024.

Msamaha

2. Kodi ya Mapato inayotokana na Kampuni ya Afcons Infrastructures Limited katika utekelezaji wa

Mkataba kati ya Dar es salaam Water Supply and Sanitation Authority na Kampuni ya Afcons Infrastructure Limited kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Mradi Wa Ukamilishaji Wa Kazi za Ukarabati wa Mtambo wa Kusafishia Maji Katika Mitambo ya Wami- Chalinze, Ujenzi wa Mtandao Mkubwa na Mdogo wa Bomba la Usambazaji Maji na Ujenzi wa Tenki Kuu za Kuhifadhia na Kusambaza Maji katika Vijiji vya Chalinze kwa kampuni ya Afcons Infrastructure Limited ya kiasi cha shilingi 642,705,377.50, kimesamehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo wake baada ya Kampuni ya Afcons Infrastructure Limited kuondolewa wajibu wa kulipa shilingi 642,705,377.50 utokanao na Mkataba ulioingiwa chini ya aya ya 2.

Dodoma,
8 April, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*